

Ushairi Huru wa Kiswahili Utashuka Lini?

Joseph Nyehita Maitaria
Chuo Kikuu cha Karatina, Kenya

Ikisiri

Makala haya yanafafanua mustakabali wa mashairi huru ya Kiswahili katika muktadha wa historia ya Ushairi wa Kiswahili. Mashairi yanayowasilishwa kwa kuzingatia arudhi za kimapokeo yamekuwepo na yana hadhira kubwa katika mataifa ya Afrika ya Mashariki hadi sasa. Mwishoni mwa miaka ya 1950 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1960, mashairi yasiyozingatia mno arudhi za kimapokeo ‘yalijitokeza’. Awali, watunzi wa mashairi haya waliwapa kibarua kigumu wakereketwa na walezi wa mashairi hayo. Hivyo, kulikuwa na jitihada za kutoa maelezo yanayohitajika kuhusu mihimili muhimu katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili. Watunzi wa ushairi huru katika miaka ya 1960 hadi 1980 walikuwa ni vijana waliobahatika kupata elimu ya darasani na kujipatia shahada katika masuala ya tahakiki za fasihi za Afrika Mashariki na kutoka sehemu nyingine ulimwenguni. Hivyo, waliotoa maelezo kuhusu ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia taratibu za uhakiki wa kinadharia. Wataalamu na isimu na wahakiki wa fasihi waliunga mkono mawazo hayo. Kadhalika, wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili (hasa katika vyuo vikuu); mashairi hayo yamekuwa ni ‘vito’. Kwa kuzingatia uwapo wamashairi huru na ya kimapokeo ni yapi yenye hadhira pana? Makala haya yanafafanua uhalisi unayoyafanya tungo za mashairi ya Kiswahili kuwa maarufu au kutokuwa maarufu katika jamii ya sasa.

Maneno Muhimu: Ushairi, Kiswahili, Historia, Mustakabali.

Utangulizi

Kihistoria, ushairi wa Kiswahili ni utanzu ambao umekuwapo na umekuwa ukitumiwa mno katika jamii za Afrika Mashariki ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi (Senkoro, 1988). Hivyo, umekuwa ni chombo cha kuwasilishia masuala muhimu katika jamii. Aidha, ni sanaa inayobuniwa na inayowasilishwa kutokana na mazingira yanayoakisi uhalisi huo. Katika uwasilishaji, mtunzi hufuma tungo za ushairi kwa kuzingatia uhuru wa kisanii na kimuundo ili kukidhi mahitaji ya sajili katika sanaa hii (Shitemi, 2010). Matukio yanayorejelewa katika

tungo za ushairi wa kiswahili ni yale yanayoshuhudiwa na wanajamii ambapo huwasilishwa kwa ubunifu kwa virejelezi vya miktadha ya utamaduni na historia ya jamii. Kupitia kwa tungo hizi, falsafa ya jamii hufafanuliwa. Mwanzoni mwa 1950 (hapa Afrika Mashariki) kulibainika kuwa, kuna baadhi ya watu waliotunga mashairi kwa kutozingatia kunga za kimapokeo. Katika mazingira haya, baadhi ya wakereketwa wa ushairi wa kimapokeo walitahadharisha kuhusu tukio hilo la ‘uchafuzi’ uliokuwa ukipenyezwa kwa makusudi kwenye tungo hizo. Katika harakati za kukabiliana naukiukaji au ‘uborongaji’ huu, taratibu za kurejelea ziliwekwa wazi. Taratibu hizo ziliwasilishwa na kuhifadhiwa kimaandishi katika *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (Abed, 1954). Kwa mantiki hii, mashairi ya Kiswahili yaliyokiuka taratibu hizo yalिकemewa na yalichukuliwa kuwa duni au za viwango vya chini. Mashairi yanayowasilishwa kwa kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo yapo hadi sasa. Kadhalika, yana hadhira ya wasomaji na wasikizaji katika mataifa ya Afrika ya Mashariki.

Katika miaka ya mwishoni mwa 1960 hadi mwanzoni mwa 1980, mashairi ambayo yamekuwa hayazingatii mno arudhi yalijitokeza na kujitafutia mwanya katika ulingo wa ushairi wa Kiswahili. M’Ngaruthi (2012) amedokeza kuwa, kuna mashairi ya aina mbili: mashairi ya arudhi na pia mashairi huru ambayo hayajifungi katika kanuni hizo za kiarudhi bali uzito zaidi ulikuwa umejikita kwenye uwasilishaji wa mawazo au fikra za mtunzi. Aidha, anakiri kuwa aina zote za mashairi ni muhimu katika nyakati za sasa. Kwa kuzingatia mwelekeo huo, M’Ngaruthi ana msimamo kuwa, tofauti iliyopo kati ya ‘ushairi wa Kiswahili’ na ‘ule wa jamii nyinginezo’ ni ya ‘kiistilahi’. Ingawa maelezo hayo ni muhimu, yanaweza kuwa ni ya kijumla mno kwa sababu ni fikira iliyojikita katika mgogoro wa ushairi uliokuwepo katika miaka ya mwishoni mwa 1960 na kushika kasi katika miaka ya 1980. Katika muktadha huu, watunzi wa mashairi huru waliwapa kibarua kigumu walezi wa mashairi ya Kiswahili yaliyozingatia arudhi. Matokeo ni kuwa, walijitahidi mno kutoa maelezo yaliyojikita katika kufafanua misingi iliyotumika kimapokeo katika uwasilishaji wa mashairi hayo. Kwa sasa, utunzi na uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili umepanuka na kuenea sana katika nchi za Afrika, japo kuna ushindani mkubwa miongoni mwa waandishi mbalimbali wa fasihi (Ngure, 2014). Hata hivyo, uwasilishaji wa mashairi kama sanaa, hutegemea jitihada, uzoefu, tajiriba, nia, makini na maelekezo ya makususdi yanayostahili. Watunzi wa mashairi huru katika miaka 1970 walikuwa ni vijana waliopata elimu ya darasa na kujizolea shahada adimu katika taaluma zinazohusu tahakiki za fasihi, masuala ya uchanganuzi wa lugha. Hivyo, walijihami kwa maelezo yaliyojikita zaidi katika taratibu za kinadharia. Baadaye, baadhi ya wahakiki wasifika wa fasihi ya Kiswahili waliunga mkono mawazo yaliyotolewa na wataalamu hao ambao pia ni watunzi wa tunzo za ushairi. Katika ulingo wa wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili; mashairi huru yalitukuzwa na yalienziwa. Hata hivyo, mashairi hayo

hayajapata hadhira pana yakilinganishwa na mashairi yanayozingatia zaidi arudhi za kimapokeo. Maswali yanayoweza kuulizwa kama vile: Ni kwa misingi gani ambapo mashairi haya yanachukuliwa kuwa ni ya kiwango cha juu ilihali hayana hadhira kubwa yakilinganishwa na mashairi yanayozingatia zaidi arudhi za kimapokeo? Hivyo, mashairi huru ya Kiswahili yatashuka lini na yatakubaliwa na hadhira pana ya Afrika Mashariki? Masuala haya yatafafanuliwa hivi punde kwa kuzingatia yafuatayo:

Kutotabirika

Katika muktadha wa Afrika ya Mashariki, mashairi huru yalikuja kwa ghafla hata kabla ya hadhira kuandaliwa kuyaokea; hawakujua wingu hili litakuja vipi. Aidha, walibaki vinywa wazi wakisubiri maelekezo bila hiari. Kwa kipindi cha sasa, mashairi hayo yametamalaki sako kwa bako na mashairi yanayozingatia arudhi kama sura mbili zinazokabiliana. Ingawa sauti ya mashairi hayo inasikika kichinichini na haijadidimia. Hata hivyo, ni vyema kuwepo na mdundo sawa la sivyo kutakuwa na cheche zizoisha kwa kulaumiana miongoni mwa watunzi na wahakiki wenye misimamo mikali wanaweza kuigawanya hadhira katika makundi mawili au zaidi ya kimielekeo; inayotengana au inayotuzwa.

Sifa Bainifu za Mashairi Huru ni Zipi?

Mashairi huru yapo na yanaendelea kutunngwa katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, jambo linaturisha bongo za watu ni: Tamrini na kunga zake ni zipi? Kila utungo wa fasihi una sifa za kuubainisha. Vipengele na utaratibu unaopasa kuzingatiwa ni vya kijumla ambapo watunzi na hadhira hujenga mitazamo yao kuhusu ushairi wa Kiswahili. Tofaiti za kiutunzi pia hushuhudiwa katika mashairi huru. Kwa mfano, kuna baadhi ya tungo hizo ambazo huwasilishwa kwa taswira dhahiri zionekanazo (tazama mashairi ya Kithaka wa Mberia katika, *Mchezo wa Karata* na *Bara Jingine*) au zile zinazowasilishwa kwa taswira za kimawazo (tazama baadhi ya mashairi ya Kezilahabi, *Kichomi*, *Karibu Ndani* na *Dhifa*; Mulokozi na Kahigi, *Mashairi ya Kisasa* na *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*). Mitindo ambayo imetumiwa katika mashairi ya watunzi hawa ni ile inayoshihi uwasilishaji wa mashairi simulizi ya Kiswahili. Hivyo, imekuwepo katika uwasilishaji wa mashairi wa Kiswahili tangu jadi ila kwa sasa imekuwa ikiangaziwa zaidi katika uhakiki wa kinadharia. Walizingatia kwa uwazi suala hili ila kosa lililofanyika ni kutowaandaa walengwa wa ushairi wa Kiswahili na matokeo yaliyoshuhudiwa ni makabiliano ambayo haikutarajiwa. Kimsingi, tungo za fasihi hususa ushairi wa Kiswahili una utaratibu na miiko katika uumbaji na uwasilishaji. Tungo zinapotoka nje ya viegemeo vya mihimili hiyo, iliawaweka wapokezi katika mazingira ya wasiwasi na kuanza kuulizauliza ambapo huweza ama kupata majibu yafaayo au yenye viwingu tata potoshi. Kwa kawaida endapo sababu zinazotolewa hakuridhisha; joto litapanda miongoni mwa hadhira. Ni wakati huo ambapo wale

waliokuwa na nia nzuri huwa hujuta kwa laiti ningalijua. Baadhi ya sifa za ushairi huru wa Kiswahili ni pamoja na:

Sifa Bainifu katika Ushairi wa Kiswahili

Kimsingi, ushairi wa Kiswahili (na tungo zote za fasihi) hutungwa kwa kuzingatia mitindo mahususi ambayo husaidia kuutambua na kuutofautisha na tanzu zingine. Ingawa kuna mashairi yanayowasilishwa kwa mitindo mbalimbali, tungo hizo zinaweza kudhihirisha mfanano na utakavyodokezwa hivi punde.

Mfanano katika Uwasilishaji

Baadhi ya wasanii wa ushairi wa Kiswahili huwa na upeo wa juu cha ubunifu na uwasilishaji wa tungo zao (Mazrui, 1988). Hii inatokana na sababu kwamba, watunzi hao huweza kuumba na kuumbua ulimwengu wao wapendavyo kwa madhumuni ya kubuni na kuunda taswira ya mandhari halisi ya kuaminika katika fikira za kuaminika kwa wasomaji na wasikilizaji (iwapo ni shairi ambalo linaghaniwa au linaloimbwa). Ushairi huu wa kimapokeo huweza kuchukuliwa kuwa una mdundo unaotokana na yale yanayoshuhudiwa katika jamii. Kwa maana hii, unahifadhi masuala ya kihistoria katika jamii (Walibora, 2007; Daiches, 1956). Hivyo, ni weledi wa kupigiwa mfano hasa kwa kubuni tungo zenye maono, ushikamano na wenye kujiweka katika muktadha wa kuhisi yale yanayohisiwa na kupitiwa na wanajamii wanzao. Iwapo wasani watakosa nidhamu ya aina hii huenda ndoto zao zikaambulia patupu. Wenye vipawa vya ubunifu na uzinduzi huwa na unafuu katika uwasilishaji wa maudhui kwa njia inagusa hisi na uchochezi wa usaili. Kadhalika, katika ubunifu na uwasilishaji wa baadhi ya masuala muhimu ya jamii yanahitaji ujasiri bali kwa kufinyanga vipengele vya lugha kwa malengo ya kuwasilisha matatizo yaliyopo katika jamii kwa kujenga tafakari inayoweza kupatanishwa na tajiriba ya watu. Kwa njia hii, ushairi unachochea akili ya hadhira kutaka kulisoma kimoyomoyo au kwa kulighani kwa ukariri. Kutokana msukumo wa mtunzi (ambao pia huweza kutokana na ujasiri), anaweza kuibua mawazo ambayo ni ya kuihamasisha, kuikosoa, kusuta na pia kuikaripia jamii. Baadhi ya watunzi wasifika wa hapo awali waliokuwa na mielekeo kama hii ni kama vile Muyaka Bin Haji Al-Ghasaniy, Mwana Kuponu, sayyid Abdulla Ahmed Nassir.

Kwa mintaarafu hii wanaotunga mashairi huru wanakuwa katika mstari wa mbele katika kuchukua hatua ya kwanza katika kujaribu mambo mapya (Wangari, 2015). Mashairi hayo yamejengeka katika muktadha wa hisi, lugha ya kutafakarisha, maudhui, mazingira, tajiriba ya maisha, historia na utamaduni. Huelezea hisi za ndani kwa kutumia lugha ya mkato na ya kipicha. Katika muktadha huo, ushairi unachochea hisi, unaamsha ari, unazindua, unamfanya mkusudiwa au hadhira kuathirika na kuridhika. Haya yanahitaji ufundi katika kuleta athari hii kwa hadhira. Lugha inayotumika inahitaji kupangwa kwa kuzingatia mpangilio na utaratibu maalum ambapo katika usomaji au usikilizaji

huibua utamu, uchungu, na uhuzunishaji. Kulingana na Mathiora na Mudachi (2007), ushairi huwasilishwa kwa mbinu zinahusisha namna miliolio ya sauti katika maneno teule yaliyopangwa kwa makusudi ili kudhibiti ujumi. Sauti hizo zinaweza kukaririwa au zikapangwa katika ruwaza za mishororo katika mashairi. Aidha, uundaji wa picha au taswira, kuvuta hisi na mvuto na kuleta mguso wa hali ya juu. Maudhui yanayosawiriwa ni yale ambayo yanatokana na uhalisi wa maisha ya watu. Kimsingi, mashairi yanayozingatia zaidi arudhi hutungwa kwa azma ya kughaniwa na kuimbwa ambapo mashairi huru huzingatia mojawapo na hasa kughaniwa. Hata yanapoghaniwa; hukerezwa kutokuwa na milingano ya sauti isiyolingana.

Isitoshе, mashairi ya Kiswahili huwa na istilahi zake za kuutambua kama vile beti (katika muktadha wa mashairi yanayozingatia zaidi arudhi) na kifungu au aya (katika muktadha wa mashairi yasiyozingatia zaidi arudhi). Hata hivyo, kilicho cha muhimu ni hoja au kiini kinachofafanuliwa kupitia kwa uteule wa maneno au kauli zinazotumka katika uwasilisaji wa hoja au mawazo.

Uzingativu Zaidi wa Masuala ya Kidhania

Kuhusu masuala yanayowasilishwa katika fasihi yanahitaji kuoana na uhalisi wa maisha ya watu kulingana na yale yanayopitiwa katika tajiriba ya watu. Hivyo, mashairi ya kimapokeo yana uhusiano wa moja kwa moja na yale yanayotendeka katika jamii. Katika ushairi huru, masuala muhimu katika jamii yanafanuliwa kifalsafa (au kinadharia) zisizoelekwa kwa urahisi. Kwa kuzingatia mweleko huu, ushairi huu unakuwa wenye ‘sauti nyingi’ katika kufikia fasiri iliyomwafaka kuhusu yale yanayowasilishwa. Katika kubainishia dhana ya ukweli Tolstoy (1975) ameelezea mshabaha huo unaojikita katika pande mbili: kwamba, si shurti kwa kila linaloshughulikiwa na msanii liwe katika muktadha wa uwezekano (au kuwezekana). Kwa mantiki hii, mtunzi ana uhuru zaidi katika kuwasilisha fikira, mawazo na maoni kuhusu mambo ambayo bado hayajashuhudiwa katika uhalisi wa maisha ya watu na kama yapo hufanuliwa kwa mifano inayoogopesha na kutisha. Tofauti na mifano inayotolewa na washairi huru ambapo maana ya ujumbe hueleweka kwa kuzingatia mukadha wa uhalisia wa utamaduni; ushairi huru nao umejikita zaidi katika ujumbe mseto wa kihadhania na uhalisia. Uhalisia huo ungekuwa unawasilishwa kwa njia inayoeleweka kwa wepesi basi hadhira kusudiwa ingepata unafuu wa kuhusisha ujumbe unaowasilishwa na maisha ya jamii.

Mbinu zinazotumika katika uwasilishaji maudhui na ujumi katika mashairi hayo huwa yamefichwa kiufundi katika katika vivingu vya maana zinazotokana na maneno yaliyotumika kwa makusudi. Fasiri ya jumbe katika mashairi hayo yanahitaji ufahamu wa kitaaluma inayojikita katika masuala ya lugha na uhakiki wa fasihi. Masuala yanayopewa kipaumbele katika mashairi huru ni kusawiri yale yalitokea jana (matukio ya historia) ili kufafanua yale yanayoshudiwa kwa sasa

na kwa pamoja matukio hayo yanajengewa muktadha wa kutabiri ya kesho au yanayotazamiwa katika maisha ya watu. Utabiri huu huweza kuwasilishwa kimaono (kwa kubashiriwa) au ya kindoto hivi. Kwa mantiki hii inawawia vigumu wana jamii kukumbatia mawazo hayo ya kibinafsi yasiyojengwa katika misingi ya kihalisia (Harland, 1999 na Daiches, 1956). Hivyo, msanii wa kazi ya fasihi ana mawazo ya kindoto au mambo yangukuwa vile ingekuwa afadhali. Aghalabu mashairi huru huwa na mwelekeo huu kama inavyodhhirishwa katika shairi la 'Bara Jingine' katika *Bara Jingine* (wa Mberia, 2001). Zaidi ya hayo, kuna kuzingatia miundo na maumbo 'yanayowezekana' japo hayapo. Jambo linalosisitizwa zaidi ni uzuri au manufaa ya kitu hicho ambacho 'kimekuwepo' na kimekuwa kikichukuliwa kiholela au nguvu yazo kupuuzwa; au ni kitu kipya ambacho hakifahamiki katika utambuzi wa wanajamii. Huu ni ushairi ambao umeingia katika jamii kwa 'mlango wa nyuma'. Tukio kama hili linapotokea, wanajamii huweza kuanza kujiuliza maswali ambapo hakuna majibu huwa ni tatizo na ya kubahatisha au kujenga viwingu vya fadhaa katika taamuli zao. Aidha, mizani ya vipimo havipo katika upeo wao. Si kwamba wanajigamba bali walikuwa wanazungumzia walichokifahamu katika utanzu huu wa ushairi wa Kiswahili. Katika mtazamo wa pili wa Tolstoy (keshatajwa) ni kwamba, tungo za fasihi huwasilisha mambo katika uhalisi wake. Hivyo, ni mambo ambayo yanaweza kufasiriwa kwa kuzingatia tajriba ya wanajamii husika; fasihi kama hizi ni za kihalisia na matumizi ya chuku huwa nafasi finyu. Hata kama chuku itatumika huwa ni ya makusudi na hutambuliwa na hadhira. Katika tungo za fasihi hii, msanii huibua hisi na mawazo yanayosadikiwa na hadhira yake. Hii inatokana na mambo muhimu yenye mshabaha wa moja kwa moja na yale yanayopo katika jamii. Msanii atakuwa anacheka na hadhira yake itakuwa inacheka; anachukizwa na hadhira yake itakuwa inachukizwa.

Fasihi yenye hadhira pana, huenziwa na huwa maarufu katika jamii. Matokeo kwa tungo hizi ni kukumbatiwa na kudumu kwazo kwa kuchukuliwa kuwa ni kazi bora. Mifano hapa ni tungo za washairi kama vile: Abdilatif Abdalla, Shaaban Robert, Muyaka Bin Haji Al- Ghasaniy, Mwana Kuponu, sayyid Abdulla Ahmed Nassir. Katika uwasilishaji, mawazo muhimu hutomelewa chuku katika uwasilishaji wa tungo hizo. Kadhalika, uketo kwamba wazo hili kwa ujumla ni kwamba, na pia ushairi fikira hizo zitashuka lini? Fikira na mawazo yaliyoundwa kutokana na daraja ya elimu ya juu ya darasa waliozipata. Maudhui ambayo yamekuwa yakiwasilishwa kwa lugha ya tasfida, lakini katika ushairi huru wa Kiswahili, makali hayo kwa ubunifu usiochujwa na ikibidi sana masuala hayo hukejeliwa. Maudhui ambayo yanahusu jana, leo na kesho. Baadhi ya masuala muhimu katika jamii yalizungumziwa na kuwasilishwa kimzaha mzaha. Kwa mfano, katika diwani ya *Kichomi* (Kezilahabi, 1974) kuna mashairi kama: 'Niachie pombe yangu' ambapo unywaji pombe unachukuliwa kuwa ndio tiba ya masaibu ya watu. Ubikra ambao ulionekana kama ni ishara ya kutulizana katika

maisha ya ujanani unachukuliwa kama adhabu na gereza ('Bikira mwenye Huzuni'), wagonjwa hawapewi ugua pole bali hushtumiwa kwa makosa walioyafanya, hawaachwi kupumua wala kuhurumiwa kwamba walijitakia wenyewe. Hizo ni nadharia za kulazimisha zisizosadifu maadili na katika mazingira ya utamaduni wa Waafrika, wanandoa kutakiwa kujichomoa kutoka kwa ndoa zao badala ya kuhimiza kuvumiliana; Kukata tamaa kwa wazee kukejeliwa na busara kutoka kwa vijana; wana mielekeo hasi na hakuna mazuri yanayopewa hadhi; wahusika wanaosifiwa ni wachawi, vichaa (Kezilahabi, 1974 na 1988). Kadhalika, fasihi ya ubwege; wanachukulia ushairi wa kimapokeo kama uliopitwa na wakati; usasa na sayansi na teknolojia inaonekana kama ni harakati zinazorudisha nyuma maendeleo katika jamii; hadhira wanaelekezwa katika kubeza maisha yao ya awali na suluhu zinazotolewa ni za uasi na kutegemea nguvu za kibinafsi badala ya nasaha katika kuendesha maisha yao na kwamba hasira si hasara kwenye shairi la 'Hasira Hasara?' katika *Chembe cha Moyo* (Mazrui, 1988). Haya yanayozungumziwa yana mwelekeo 'hatari' na yenye kuupotosha uhalisi wa maisha Hivyo mashairi ambayo hayazingatii arudhi, huwa vivuli vifu katika maana inayowasilishwa na mashairi yanayozingatia arudhi katika uwasilishaji wake huwa yenye maweko yake.

Ushairi wa Kiswahili kama Mali ya Umma au ya Kibinafsi?

Kauli kama vile: Ushairi una 'wenyewe' (ushairi unazingatia arudhi za kimapokeo) wa 'mwenyewe' (ushairi huru); na baadhi ya watu katika jamii walifikia misimamo ya kijumla kuwa: 'wale si wetu.' Mashairi yanayozingatia zaidi arudhi yana wenyewe ambao huyashikilia yasadondoke. Walijichukulia kuwa ni jicho na mwokozi wa umma! Aghalabu, mashairi haya yanapatikana vitabuni na haujapata mwanya wa kujitokeza hadharani ili kukutana na umma. Katika kutunga ushairi wa Kiswahili (na kama ilivyo katika tanzu zote za fasihi) kunalenga zaidi mwitikio wa wapokezi kama vile wasomaji na wasikilizaji na wala si watunzi hawajitungii (Alembi, 1999; Senkoro, 1988).

Kutokana na namna unavyopokelewa, ushairi unaozingatia mno arudhi, umejijengea umaarufu zaidi mashinani na kuwa 'mlinzi' na 'sauti' ya umma (hadhira pana katika jamii). Sababu zenyewe zinaweza kuorodheshwa hapa: uzingatiaji wa urasimu uliokuwepo katika uwasilishaji wa tungo hizo; lugha inayoeleweka kwa urahisi; ujumi umedhibitiwa na kuacha athari kubwa katika hadhira. katika muktadha huu, husomwa na hukaririwa kwa wote katika jamii bila kujali sana kiwango cha elimu ya hadhira; maudhui na mtindo hufungamanishwa na kile kinachoelezwa kwa kuzingatia jinsi kinavyoelezwa. Hivyo, ushairi huu umejijengea utamaduni pendwa kwa kuwasilisha masuala ambayo yanafungamana zaidi na maisha ya watu (Wafula, 2007; Barber, 1997). Hata hivyo, dhana ya 'mali ya umma' kwa kurejelea baadhi tungo za ushairi wa Kiswahili una matatizo yake. Wanaoshikilia msimamo huu wamekuwa wakistahabu kuusheheneza sifa zile zile za tangu jadi na kuielekeza kidole ngome

hii kutoka nje inachukuliwa kuwa ni dharau kwa wanajamii. Isitoshe, baadhi ya semi na kauli zimekuwa zikitumika kwa sasa ni vito vya busara zinatekeleza dhima katika usemezano, maingiliano na mijadala yenye kubeba busara ya jamii pana. Iwapo pana haja ya kuwepo kwa mabadiliko katika uwasilishaji wa maelekezo ya busara katika jamii; hutafutiwa suluhu kutoka kwa ‘ngoma ya ndani’ katika jamii. Hawatawaliwi kwa mtazamo nje kuulinganisha na namna au mbinu zinazoitumika katika uwasilishaji wa mashairi hayo. Hii ni imani ambayo ilihitaji kufanyiwa mabadiliko; mabadiliko hayo hayakufaa kuandamwa kwa ghafla.

Harakati za Makusudi katika Kuupigia Debe Ushairi wa Kimapkeo

Katika matoleo ya magazeti ya Kiswahili yaliyopo katika baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki kama vile *Taifa Leo* kuna safu za mashairi (Nchini Kenya kuna *Taifa Leo* la Jumamosi na *Taifa Jumapili* na nchini Tanzania kuna *Majira*, *Mtanzania*, *Mwananchi*, *Nipashe*, *Mzalendo* na *Uhuru*,). Katika mashairi hayo, yale yanachapukiwa mno ni yale yanayofuata arudhi. Hivi si kusema kuwa mashairi huru hayapo, bali kama yapo katika matoleo ya magazeti ya Kiswahili ni machache mno. Watunzi wengi wanaoshriki katika safu hizi huwa ni jukwaa la kusemezana na kujibizana kuhusu masuala yanayowahusu. Kadhalika, mashindano ya wanafunzi wa shule za msingi na upili; mashairi ya kiarudhi ndiyo yanayotumiwa kama chombo cha kutumbuiza na kuwakalisha kitako wasikilizaji.

Idhaa za radio hazikuachwa nyuma; nchini Kenya kuna *Radio Citizen*, *Radio Maisha* na *Kenya Broadcasting Corporation* na Tanzania kuna *Tanzania Broadcasting Corporation*, *Radio Free Africa* pamoja na runinga za mashirika hayo hupeperusha vipindi maalumu vya mashairi ambayo kuzingatia arudhi. Vipindi hivyo hutumiwa kama ‘vipumuo na viliwazo’ au vitumbuizo vya kuwaweka kitako wasikilizaji. Nguvu ya ndani katika mashairi haya ni kuwa, watunzi hao hawajashurutishwa bali hutungwa na huwasilishwa kwa raha za watunzi wenyewe. Mashairi huru machache ambayo yamepata kuchapishwa katika matbaa lakini kinachobainika ni kuwa baadhi ya diwani hizo zimesheheni tungo chache za mashairi huru ya kiwango cha juu na mengi huwa ni ya kulazimishwa na kutojali. Hii inatokana na ukosefu wa ufahamu wa taratibu zinapaswa kuzingatiwa katika rubaa ya wahariri. Jambbo hili pia limeathiri ufundishaji wa ushairi huu katika ngazi mbalimbali za elimu hapa Afrika Mashariki. Isitoshe, mashairi huru mengi ambayo yamechapishwa katika matbaa za kibinafsi au kugharimia uchapishaji ambapo yana makosa mengi yaliyowazi na ujumi uliofundwa huwa haujitokezi kwa uwazi (hapa matbaa hizo za kibinafsi hazitatajwa ila kilicho cha muhimu ni kuwa, mashairi yenye mwelekeo huo yapo). Kutokana na mahitaji ya soko na idadi ya hadhira finyu ya mashairi haya; uamuzi wa mwisho huwa unaafikiwa na wenye kumiliki matbaa za uchapishaji zilizopo.

Ukosefu wa Istilahi katika Utambuizi na Uainishaji wa Ushairi Huru

Katika ushairi unaozingatia arudhi huwa na sifa na istilahi bainifu: mashairi yenye idadi maalumu ya mizani na mishororo, ruwaza ya vina, kibwagizo na viishilio, unaofuta utaratibu katika utiririshaji wa mawazo miongoni mwa mengine. Swali hapa ni: je mashairi huru yana kunga zake mahususi katika uwasilishaji wake? Mashairi hayo yana maumbo maalumu? Mahadhi na muundo hushughulikiwa vipi katika katika mashairi haya? Maelezo kuhusu masuala hayo yametolewa na baadhi ya wahakiki wa fasihi kuhusu utungo huu.

Hofu Inayonyemelea Baadhi ya Watunzi wa Ushairi wa Kiswahili kwa sasa

Baadhi ya watunzi ambao ni wasomi miongoni mwa wataalamu na wahakiki wa fasihi, (ingawa walifahamu nguvu ya ushairi huru) ‘wanatumia kwa mbali’ arudhi hizo katika uwasilishaji wa mashairi yao. Walishtuka ushairi huu ulipojitokeza na hadhira ikaanza kuuchangamkia. Hivyo, yalichukuliwa kuwa ‘hatari’ kwa ushairi wa Kiswahili uliozowewa; hawakupewa nafasi. Walichokijali zaidi ni kutambuliwa na kujihusisha na kundi maarufu katika tasnia ya ushairi ulio maarufu katika jamii (Taz. diwani za mashairi ya Kiswahili kama *Miale ya Uzalendo, Chembe cha Moyo, Jicho la Ndani* na *Wasakatonge*). Hofu hii inajitokeza pia miongoni mwa matbaa za uchapishaji ambapo inafahamika kuwa hadhira ya ushairi huu ni finyu.

Ushairi Huru kama Utanzu wa Majaribio na Utafiti

Kuwa kuzingatia kasi ya watunzi wa ushairi wa Kiswahili, katika miaka ya 1960 hadi wakati huu wa sasa baadhi ya watafiti wamepata uwanja wa ulinganishaji na utofautishaji wa mashairi katika jamii mbalimbali. Kutokana na namna mashairi ya Kiswahili yanavyowasilishwa kwa mitindo mbalimbali, kumekuwa na mitazamo ya kimaono kuhusu masuala ya kiutuzi na usomaji wa mikakati ya kutegemewa. Dhana ya ‘bora ushairi’ itakuwa imedhibitiwa na kuwepo kwa ‘ushairi bora’. Hivyo, walitaka ushairi kubainishwa kwa uelekezaji wa mbinu za ‘kisasa’ kupitia uwasilishaji unaojikita katika mitindo ‘mipya’ ya fasihi ambayo tayari imefanyiwa utafiti katika ngazi za kimataifa (Wafula na Njogu, 2007; Njogu, 2004). Katika muktadha huo, vigezo vilivyokuwa vikitumiwa kwa uelekeo wa kijumla vingaliweza kutazamwa upya na kubainishwa ili kuweza kuanishwa kwa utaratibu wa unaozingatia mbinu za kisayansi. Isitoshe, ushairi wa Kiswahili ungeweza kulinganishwa na mashairi kutoka jamii za hapa Afrika Mashariki hata kupitia kwa ushairi wa mataifa ya kigeni ambapo mazingira tofauti yaliweza kuibua tungo hizo Hapa ifahamike kuwa watunzi hao wa awali wa ushairi huru walikuwa wana ujuzi wa kutosha katika taaluma ya lugha na fasihi. Kimsingi, hakuna ila kukumbatia mawazo kutoka ugenini kama ilivyochukuliwa na watunzi wa ushairi wa Kimapokeo; muhimu ni kuchuja na kuhusisha yale yanayoweza kuuboresha ushairi huu. Kwa mtazamo huu, watunzi na wasomaji wa ushairi wa Kiswahili wameweza kupanua mawazo yao kwa

kufikiria nje ya mipaka iliyo zowewa. Ni kweli kwamba kila utanzu una utaratibu na miiko yake lakini pia walitaka watunzi wavifahamu vipengele muhimu vinavyohusishwa katika uwasilishaji na wasomaji wanatarajiwa kuwa makini wakati wa usomaji wao ambapo hawatakuwa wakikubali tu kimazoea yale wanayowasilishiwa bali kuwa na vigezo (vichujio) katika kuukabili ushairi na kufikia maamuzi ya kutegemewa kuhusu hoja zinazowasilishwa kwa jicho pembuzi la kiuhakiki. Japo ushairi huru wa Kiswahili ulijitokeza wazi katika miaka ya 1960 tena kwa sura au maumbo ya nje yasiyoeleweka na yasiyopendeza; kupendeza kwake usetiriwa kwa fani tele na uwasilishaji wa kiufundi wa ndani kwa ndani katika mashairi hayo. Katika mazingira haya, ushairi wa Kiswahili utakuwa umevuka mipaka ya kuchukuliwa kiujumla na kushughulikiwa kitaaluma zaidi. Kwa sababu, watunzi watakuwa wamefunuliwa namna mbalimbali katika kuufahamu zaidi ushairi huo kutokana na sifa za kisayansi. Kwa kipindi cha sasa, ushairi wa Kiswahili unafafanuliwa kwa vigezo vinavyozalika kwa uchunguzi wa aina ya fasihi inayozingatiwa. Ingawa safari ya washairi huru ilikuwa ya kukatisha tamaa kwa kupigiwa upatu na umma wa watu ambao walikuwa na mawazo kuwa ushairi wao ‘umehujumiwa’, ‘umeshafuliwa’ au ‘umetiwa najisi’; ndoto yao haikuyeyuka bali walisonga mbele kwa ‘atakayesikia na asikie na ‘asiyetaka asitake’ kusikia. Misimamo kama hii ndio inapiga hatua za kimaendeleo katika ushairi wa Kiswahili.

Dhana ya Kuurudisha Ushairi kwa Umma

Ingawa utaratibu katika uwasilishaji wa ushairi huru wa Kiswahili haukuanza katika miaka ya 1960; ni mtindo ambao umekuwepo katika tamaduni mbalimbali za tangu azali katika Afrika Mashariki na hasa katika ushairi simulizi na nyimbo (tazama *Mashairi ya Muyaka*; mashairi katika diwani za Shaaban Robert; *Al-Inkishafi*; *Utenzi wa Mwanakupona* na hata nyimbo zilizowasilishwa ana kwa ana katika sherehe maalumu katika jamii). Jamii ndio hutungiwa na huwa na vigezo vya kutambua mwelekeo unaohitajika na hatima ya tungo za fasihi (ushairi wa Kiswahili ukiwemo); wanajamii ndio wanaoishi maisha yanayotawaliwa na utamaduni wao. Hivyo, wanajamii hao ndio wanaoathiri na kuathiriwa na maisha hayo. Katika muktadha huu, baadhi ya maswali yanayoweza kuulizwa: ushairi ni sanaa (au ushairi) wa nani? Akina nani walioliteua kundi hili kuwakilisha jamii au umma? Umma huu ulikuwa upi? Kadhalika, watundu hao walipoanza kuzungumzia kuwa katika ushairi katika mataifa mengine ya kilimwengu ulishirikisha mitindo yote miwili: arudhi na huru. Mawazo hayo yalichukuliwa kuwa ni uchafuzi wa kunga katika utanzu wa ushairi uliokuwa umezowewa katika jamii ya Waswahili. Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1960 baadhi ya wasomi wa elimu ya kigeni na hasa hao ‘watundu watatu’ walipoanza kuzungumzia kwa hamasa suala hili kwa kuzingatia kuwa baadhi ya watunzi walikuwa walikuwa hawatilii maanani katika uwasilishaji wa tungo zao. Tatizo ni kwamba, walianza kwa kushambulia kwa makeke na mabezo yasiyohitajika lugha ngumu iliyojaa

maswala ya isimu katika uchambuzi na uhakiki wake. Ushairi wa kuwafikia watu wa kawaida? Nani ambaye angependa kuhusishwa na watu wa kawaida. kuna ushairi huru huzingatia zaidi dhana ya uhamishaji wa ujumbe na kuupatanisha na hali halisi au matukio halisi. Hulenga aina moja ya hadhira ambapo wasomi ambao ni watunzi husemezana wao kwa wao na katika ushairi wa kimapokeo hukata pande mbili (wasomi na watu wa kawaida). Makabiliano ya kifalsa kwa lugha ya mafumbo. Mashairi hayo ni nadra kuchapishwa na havinunuliwi ila na kundi dogo la wasomi wa ngazi za juu kama vile wahadhiri, wahakiki wa isimu na fasihi wenye kiwango cha juu cha uchambuzi wa matini hizo. Wanafunzi wa ngazi za chini wanataka njia ya mkato tu na mashairi hayo hayakupata pahali pa kuwaweka. Baadhi ya mashairi hayohuwa ni sentensi moja ambayo hajaakfishwa na mahadhi yake yanaweza kueleweka na kuhisika kupitia kwa usomaji wa sauti. Ni ushairi unaowanyima uhondo akina yakhe kwa kuwabagua badala ya kuhusisha. ni ushairi unaofahamisha na kuchochea tafakuri badala ya kubainisha taswira ya mambo jinsi yalivyo. Waamuzi wa umashuhuri wa ushairi wa Kiswahili kimsingi ni wasomaji au hadhira.

Walimu Wachache Wanaomudu kunga za Uwasilishaji wa Ushairi Huru

Kuna mwelekeo kwamba ushairi ni mgumu na haupendwi na walimu ambao pia wamewikwa jukumu la kuwatarisha wanafunzi wa shule za upili kwa mtihani wao wa kitaifa. Katika ufanzaji mwafaka wa mashairi ya Kiswahili ni muhimu papewe na mwongozo mwema kwa watarishaji na watarishwaji. Usomaji wa kibinafsi ni mchache mno, hauendelezi utamaduni wa usomaji miongoni mwa wanafunzi wala walimu; baada ya masomo ya darasa huwa ndio mwisho. Maendeleo ya ushairi huru wa Kiswahili unaingia katika njia panda. Hakuna ajuaye ataiandama njia gani: njia tata isiyoeleweka au ile iliyonyooka inayofahamika? Matokeo ni kwamba, wanafunzi hao huwa hawakujengewa muktadha wa 'kutenga na kuhusisha' vipengele husishwa katika uwasilishaji wa ushairi huu. Baadhi ya wanafunzi katika viwango mbalimbali kuanzia shule za upili hadi vyuo vikuu huwa na hofu wanapozingatia mada zinazohusu ushairi kwa ujumla; hofu zaidi ni katika ushairi huru wa Kiswahili. Ni kama wanashurutishwa kusoma mashairi huru ya Kiswahili kwa sababu ya mtihani na baada ya hapo; husahau yaliyopita na kuandama masuala mengine ya maisha. Wafuasi hao wanaachwa wakichechema na kutapatapa katika bahari hii ya ushairi huru wa Kiswahili. Tatizo kubwa zaidi hapa ni, sasa uhaba wa tungo hizo na diwani katika maduka ya vitabu.

Utaifa na Umataifa wa Ushairi wa Kiswahili

Kufananisha na ushairi wa mataifa¹ ya Afrika Mashariki na kwengineko . Ukweli ni kwamba wanaotunga na kuwapendekeza watu yanayotarajiwa kufuatwa ni wasomi na wataalamu wa lugha na fasihi kama vile *Kichomi* (Kezilahabi, 1974) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Kahigi na Mulokozi, 1979), *Bara Jingine* (wa Mberia, 2001), *Tamthilia ya Maisha* (Wamitila, Mh. 2005) na baadaye *Jicho la Ndani* (Mohamed, 2002). Hawa walikuwa wamesimama ‘mlimani’ wakiwaangalia walio chini. Walikuwa na maono katika kuukuza na kuuendeleza ushairi wa Kiswahili kwa ujumla lakini namna walivyojitokeza kwa kumbo za fujo ndivyo walivorudi. Kabla ya lugha ya Kiswahili kuenea na kutumiwa kwa matumizi mapana, ushairi wa Kiswahili ulikuwa ni utungo uliokuwa umekita mizizi katika jamii ya Waswahili lakini baabaye lugha hiyo pamoja na ushairi wake ulikuwa ni kitambulisho cha jamii pana ya wenyeji wa Afrika Mashariki.

Uelekezaji Usiokuwa na Subira

Watunzi waushairi huru walikuwa na ari ya kubainisha na kuhalalisha hoja zao kuhusu baadhi ya vipengele muhimu katika ushairi wa Kiswahili. Kulingana na yale waliyokuwa wameyapata katika usomi wao kuhusu fasihi linganishi za kimataifa kwa kuzingatia miundo na maumbo ya ushairi kwa ujumla. Kwa nini kila upande ulikuwa upinzani wenye hasira? Mawazo ya washairi huru yalikuja kwa mikiki na vishindo. Kimsingi, mabadiliko yalitarajiwa kutekelezwa mara moja hata kama yalikuwa na nia njema ya kustawisha ushairi wa Kiswahili. Ingawa walioshikilia ushairi huru walikuwa na mawazo muhimu ya kutaka kuuweka utanzu huu katika ngazi nyingine, hawakuwa na subira, walijitenga kwa kujipiga vifua, kuusuta ushairi huo kwa kalamu ‘zilizopayuzwa’ na kipaza sauti za ‘kashfa’. Kwa upande wao walijichukulia kuwa wao ndio wenye ‘ufunguo’, ‘wanamaendeleo’, ‘wanausasa’, ‘wanamadiliko’, na ‘wanamapinduzi’. Hofu ilitanda kuwa kuna njama ya watundu wanaoelekezwa kwa malengo ya tamaa kutaka kuuvunja ushairi ambao umekuwa ni ngome ya kuhifadhi na kufafanua masuala muhimu katika utamaduni wa jamii. Hapa ieleweke kuwa, ngome iliyozoeleka huwa ni vigumu kuiingilia na kuivunja. Hivyo, ushairi huru ulikuwa kama ‘sumu’ inayomwaywa na watunzi hayo wenye mielekeo hiyo walichukuliwa kuwa ni wavamizi wa maeneo matakatifu. Hali hii ilikuwa ya vuta nikuvute ambapo kama sulusu ilitolewa; ilikuwa imegubikwa kwa wingu la tuhuma miongoni mwa washika dau hao. Upinzani endelevu katika ushairi ni ule

¹Dhana ya ‘mataifa’ hapa inamaanisha maeneo au jamii pana ambazo si za Uswahilini. Hii inatokana na matumizi pana ya lugha ya Kiswahili na ushairi ambao kwa sasa unamtazamo unaojumuisha jamii mbalimbali zaidi ya jamii ya Waswahili.

unaokosoa kwa kutoa suluhisho kwa kuzingatia changamoto zinazouzonga wakati huo. Kezilahabi (1983) anashikilia kuwa mgongano kati ya wanamapokeo na wanapinduzi hauwezi kuepukika. Je, wanapinduzi walitumia mikakati gani katika kufafanulia hoja zao kuhusu ushairi wa Kiswahili? Mwongozo mwafaka ungekuwa ni kushiriki maono na matarajio sawa ambayo yangeleta maridhiano.

Kuhusu suala hili Mahmoud Ahmed Abdul Kadir (almaarufu *Ustadhi Mao*) ambaye ni mtunzi maarufu kutoka Lamu, ameeleza kuwa: washairi wa kimapokeo wanatambua uwepo wa washairi huru na umaarufu wa wa tungo hizo unatokana na ambavyo kuzingatia baadhi ya arudhi za ushairi wa kimapokeo². Aidha, washairi huru walikuwa wakijijengea mazingira ya kujiweka katika tabaka tofauti na lile linalozingatia zaidi arudhi katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Waliandama dhamiri yao bila ya kugeza athari ya kauli zao. Hivyo, washairi waliozingatia zaidi arudhi walichukuliwa kuwa ni kundi la ‘mahafidhina’, ‘tabaka lisilotaka mabadiliko’, ‘tabaka la kupazia sauti ya wazee’ na ‘tabaka la watunzi ambao hawajaelimika’. Katika muktadha wa juhudi za kukabiliana na tishio hili, jukwaa la kutoa cheche za matamshi liliandaliwa ambapo hajakufaa katika uelekezaji wala kujali hadhira. Mazingira hayo hayakuwa yamejikita katika kuleta maridhiano na washairi huru walihumiwa kuwa walitaka kuivamia, kuiingilia na kuitema ngome ya ‘wenyewe’ iliyojengwa kwa kujifunza na subira ya miaka mingi hadi kufikia vile ulivyokuwa katika miaka hiyo ya 1960 (na kwa kiasi fulani mpaka sasa) ilifahamika kuwa ni himaya ya umma. Wahakiki wa kifasihi (ambao pia ni watunzi wa ushairi huu) na watunzi wa ushairi huru walihitaji kuwa na moyo ambao uwazi katika kukubali walakini wao na kujali mawazo ya upande mwingine (kulingana na yale waliyokuwa yale yaliyokuwa yakielezwa na washairi wanaouenzi ushairi unaozingatia arudhi katika uwasilishaji wake). Japo walikuwa na mawazo elekevu, walitarajiwa kutumia busara ya kudhibiti jazba ya mivutano na mori waliokuwa nao katika kubainisha hali. Uhalisi uliokuwepo katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili wa wakati huo na wafuasi wa ushairi wa kimapokeo wangeelewa. Hivyo, hawakupaswa kuingiwa na kiburi katika kuwasilisha hoja zao pasi na kuwabeza wnzao wanaoshiriki utunzi wa tungo za ushairi wa Kiswahili. Dosari hapa ilitokana na dharura iliyokuwepo ya kutaka kuhalalisha mawazo

²Haya yanatokana na mahojiano ya msanii huyu yanayopatikana katika safu ya ‘Gwiji wetu’ kwenye Gazeti la *Taifa Leo* (tarehe 4. 3. 2015, uk. 17.). Mzee Mahmoud Ahmed Abdul Kadir anakiri kuwa yeye amekuwa akitunga mashairi ya Kiswahili kwa miaka mingi kwa kuzingatia arudhi arudhi za kimapokeo; ushairi huru pia umepata kiasi fulani cha wafua kutokana na kushirikishwa kwa kiwango fulani cha arudhi katika uwasilishaji wake.

yaliyoegemea mielekeo ya kutotka kushindwa. Hii ndio sababu ya kuwepo kwa juhudi za makabiliano ya kurushiana maneno makali. Hakukuwepo na majukwaa ya uwajibikakaji katika kuanzisha mazungumzo ya ana kwa ana kwa malengo ya kushirikisha juhudi za pande hizo mbili. Katika miaka ya mwishoni mwa 1980, walibaini kosa lilitokana na kuandama hasira ya haraka ambapo hadhira haikurejeshwa katika kuzingatia mihimili ya ushairi lakini wakati huo tayari athari ya matamshi yao ya awali yalikuwa yamekwisha kuenea na maji yakimwagika hayazoleki na yakizoleka huwa na taka. Chuki na tuhuma tayari ilikuwa imetanda na kujengeka katika pande hizo zinazokinzana. Kila kikundi kikivutia upande wake na hakuna aliyetaka kuambizwa wala kusemezana. Majukwaa ya kujadiliana na kusemezana hayakuwepo na waliohimiza na waliohimizwa ilikuwa ni kero za kutoana kwa cheche za lawama.

Kujitetea huko kwa washairi huru hakukusaidia katika kuelekeza katika kupata suluhu ya kudumu. Hili ni jambo ambalo bado linaendelea chini kwa chini katika baadhi ya wasomi na wahakiki wa fasihi katika taasisi za elimu kama vile vyyo vikuu. Kutokana na elimu juu ambayo washairi huru waliipata ughaibuni walitaka sauti yao kusikika ili waonekane na kutambuliwa katika sanaa hii. Hilo halikuridhiwa, kwani walisukumwa kuchukua hatua ya kuwashikisha adabu hao ‘watoto watundu’ kwa kupigapiga mijeledi kabla ‘sumu’ hiyo kusambaa, kuenea na kuwaathiri ‘watoto watiifu’ katika jamii.

Ushairi uliozingatia arudhi ulikuwa ni kama sanaa inayoumbiwa watu fulani, hakuna wengine nje ya watu hao wanaoweza kufahamu mizungu ya sanaa hii. Hivi ni vita vya kujitafutia ubabe katika ulingo huu wa ushairi wa Kiswahili. Hii lilitokana na msukumo wa kujitakia kutambuliwa ambapo suluhu iliyotokana na mwelekeo wa hasira na wakati huo huo wakawa wanaeneza mawazo hayo kwa wafuasi wao wengine. Hata kama kauli zilizotolewa zilikuwa na busara ya ndani kwa ndani; hakuna aliyetaka kushika mawli-matatu ya mwenziwe. Tatizo kuu hapa lilikuwa ni ukosefu wa juhudi za pamoja. Waliokwisha kuonja mawazo hayo, walikuwa wenye mwelekeo unaoweza kufananishwa na tunda linaloning’ia isijulikane kama limeiva au bado ni tosa. Hawakuwa na waelekezaji wa kuwaongoza na wameachwa kuanza kupiga mbizi au kuendelea na safari katika bahari kuu wasiojua. Kuna haja ya kutathmini kina chake kabla ya kuianza au kuendelea na safari. Wameachiliwa kucheza ngoma wasiojua fika ila kwa kutaka kujihusisha na ushairi huo. Wale waliokwisha kubobea katika sanaa hii na kupata tajriba ya kutosha ndio hao hao. Ni ushairi ambao umewaacha watunzi katika hali ya kujilea: kila mmoja ana namna ya uwasilishaji: Kithaka, Kahigi na Mulokozi, Kezilahabi.

Mabadiliko ambayo yalitarajiwa kutekelezwa kwa wakati huo huo. Hawakubainisha azma yao kabla. Ingawa ushairi huru ulikuwa wenye pumzi ‘mpya’, pumzi hiyo ilikuja kama kimbunga. Walianza kusesitiza na wala si kweka kikao cha kupitisha busara na hekima iliyoficha katika tungo hizo. Walianza kwa

kutunga mashairi na ikachukua muda mrefu ndipo baadhi ya tahakiki zikaanza ktokea katika majarida ya *Kioo cha Lugha, Kiswahili, Mulika* na baadhi ya tahakiki za ushairi kama vile *Nadharia: Tahakiki ya Ushairi wa Kiswahili* (Senkoro, 1988) na baadhi ya waunzi walianza kutanguliza katika diwani zao kwa ufafanuzi mfupi wa ushairi huru kama inavyobainishwa katika *Kunga za Ushairi na Diwani yetu* (Kahigi na Mulokozi, 1979). ‘Baba’ au wa ushairi huu kwa sasa ni mzee. Watunzi ambao waliokuwa na nia ya kupata uekezi muhimu walioachwa kama watoto wachanga waliokuwa wakitambaa; hawajainuka na kukimbia sembuse kutembea. Wafuasi wa ushairi huu waliishi katika kivuli cha waanzilishi wao kama ilivyokuwa katika ushairi wa kimapokeo. Hao waanzilishi, wamebaki katika maziwa makuu wanaoagelea na kusemezana wao kwa wao. Mawazo yetu ni kwamba maandalizi hayo hawakutendewa haki. Inapolinganishwa na ushairi unaozingatia zaidi arudhi, hadhira yake ilikuwa inafahamu kimapokeo kuhusu sifa na vipengele vya msingi vilivyohitajika katika uwasilishaji wa ushairi huu.

Ushairi wa Masafa Mafupi

Wachache ndio hutunga tungo chache na baada ya hapo hupotea katika ulingo huu (Mifano hapa ni kama vile diwani za *Tunu ya Ushairi* (Arege-Mhar. 2014) na *Tamthilia ya Maisha* (Wamitila- Mhar- 2005). Baadhi ya watunzi hawana mwelekeo na hawapati ari wala hamasa za kuendelea katika miradi ya tungo hizi. Aidha, suala la uhuru wa kisanaa katika uhairihuru wa Kiswahili ulichukuliwa vibaya na baadhi ya watu. Mfano hapa ni masuala ya uwasilishaji kama vile ridhimu (mahadhi), lugha iliyokuwa ikitumiwa, hali inayojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya mambo hayo (ingawa yalikuwa muhimu katika kuufahamu zaidi ushairi wa Kiswahili) yalielezwa kwa lugha ngumu ya kinadharia ambapo haikuweza kueleweka kwa urahisi miongoi mwa hadhira.

Hadhira pana ya ushairi wa Kiswahili haikutengewa wasaa wa kuhusishwa vilivyo kuhusu mbinu na mitindo iliyokuwa inapendekezwa. Isitoshe, mawazo yao yalikuwa ya kulamisha na kuchukuliwa kuwa ni tiba badala ya mapendekezo. Kama ni mapendekezo yalizungumziwa katika ngazi za juu za kiusomi na mijadala ilikuwa kuko huko katika vilele vya milima. katika mazingira haya, mawazo yao hayakueweka vizuri kwa wale wasiokuwa na upeo wa kadri (au wale waliokuwa wakiuenzi ushairi huo katika mapokeo ya jamii au wale waliokuwa wakitunga kwa uelekezi wa vipawa vyao usanii) kuhusu vipengele vyake vya kiutunzi na ubainishaji wa maudhui yanayowasilishwa (kama ilivyoielezwa hapo awali kuwa maudhui yanayoshulikiwa zaidi ni yale ya kidhahania). Tatizo lingine linaloukabili ushairi huru ni kuwa, matibaa zilizopo katika Afrika Mashariki zimo mbioni katika biashara ya vitabu vinavyouzwa kwa haraka iwezekanavyo na hawana maghala ya kuhifadhi vitabu visivyonunulika. Hadhira kubwa hununua diwani zilizopo za mashairi haya hasa wa ngazi juu za kiusomi.

Katika daraja za chini za kiusomi kama vile katika shule za upili au vyo vya walimu; wanafunzi wanapohitimisha masomo yao ya darasa huwa hawana haja ya kudurusu diwani hizo na zinakuwa ni mapambo katika mashaka ya kibinafsi ya vitabu. Endapo matbaa huchapisha diwani hizi, huwa si idadi ya haja. Nani anayetarajiwa kuchapisha miswada ya diwani au tungo za fasihi ambazo hazina wateja (wasomaji) au wanunuzi? Hivyo, uchapishaji huo wa mashairi huru huwa ni mdogo mno na gharama ni ya juu mno (Ngure, 2014). Agahalabu, maswali ambayo wasimamizi wa matbaa hujiuliza ni: nani atakayenunua diwani za mashairi huru? Vitabu vinavyonunuliwa kwa haraka ni vile vinavyoambatana na mahitaji ya wakuza mitaala kama vile KICD. Mwanzoni (wale ambao kwa sasa ni wazee) walikuwa na imani kuwa hatimaye wangepata mabadiliko. Lakini malumbano yaliharibu mambo kwa kuwatenganihsha na hadhira pana. Aidha, hawakujua ingechukuliwa vipi na hadhira.

Suala la Lugha Itumikayo katika Uwasilishaji wa Ushairi Huru

Mnato na mizungu inayozingatiwa katika uwasilishaji wa ushairi wa kiswahili (Tazama baadhi ya mashairi hayo katika diwani zifuatazo: *Diwani ya Midulu* (Sengo, 2010), *Waja Leo: Diwani ya Mashairi* (Walibora – mhar., 2012), *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973), *Diwani ya Massamba* (Massamba, 1976), *Kina cha Maisha* na *'Sikate Tamaa* (Mohamed, 1984 na 1980 mtawalia), *Malenga wa Vumba* (Amana, 1983). Watunzi wa mashairi haya hawakurusu uvunjaji wa sarufi ambao ni nguzo kuu katika kuibua ujumi katika usemezano baina ya fanani na hadhira. Hapa izingatiwe kuwa ujumi katika ushahi wa Kiswahili hutamakani kwa mbwembwe za lugha. Hivyo, miundo hiyo ya lugha imekuwa ikivua misingi na mihimili ya ushairi wa Kiswahili hasa katika kuibua ujumi wake. Aidha, mashairi huru yamesheheni mikatale ya uzingativu wa masharti ya sarufi ambao huuviza ule mvuto unaoumua ujumi. Isitoshe, katika ushairi huo kuna uhuru mwingi wa kimtindo usiodhitiwa na matokeo ni kuuvika ugeni katika uwasilishaji wa ushairi huu. Katika mashairi ya kimapokeo, uhuru huo upo lakini umedhibitwa na istilahi zinazoashiria uhuru huo zipo na zinaeleweka kama vile 'tabdila', 'mazida', 'ikisari', 'mashairi ya pindu' 'msuko', 'idadi ya mishororo', vina vya ndani na vya nje katika beti inajulikana na majina ya aina ya mashairi hayo ni jambo lililofahamika katika bongo za watu. Wale watunzi mashuhuri wa zama waliweza kuweka misingi hiyo ya kurejelea na tungo zao zilikuwa mifano ya kuigwa. Mvuto katika ushairi ili uguse hadhira katika yale wanayoyasema kwa kuona yanayoyasema. Kwa maana hii, watunzi hao huelezea hisi za ndani kwa lugha ya mkato au ufupi kwa maneno yaliyopangwa kwa uangalifu. Lugha ya mnato kwa utamu wa mneno. Hii ni lugha ambayo huchukuliwa kuwa yenye nguvu ya kuibulia ujumi katika uwasilishaji. Mashairi anapotunga tungo zake huifikiria na kuitilia maanani hadhira kusudiwa. Hii haimaanishi kuwa, lugha inayotumiwa ngumu au isiyoeleweka. Ugumu huo ni jambo la mjadala, kwa

ambavyo hutegemea kiwango cha uchambuzi cha hadhira. Mtumizi ya lugha ya kawaida amabayo haina urasimi.

Utata na Fasiri wa Dhana zinazohusishwa katika Ushairi

Fasiri mbalimbali zimetolewa kwa kuzingatia mrengo wanaoutilia maanani. Miongoni mwa wafasiri hao ni: Ablilatif Abdalla, Euphrase Kezilahabi, F.E.M.K. Senkoro, Joseph Mayoka, A. Mazrui, K. K. Kahigi na M. M. Mulokozi. Hakujakuwa na msimamo mmoja kutokana na fasiri hizo. Kulingana na Babusa³ ni kuwa, mpaka wakati huu wa sasa hakujakuwa na msimamo mmoja kuhusu maana ya ushairi wa Kiswahili bado ni changamoto hata miongoni mwa watunzi na wahakiki wa fasihi. Kadhalika, Nabhany katika (Said, 2012) ana mawazo kwamba, utungo (ushairi wa Kiswahili) lazima na sifa saba zifuatazo: bahari, kina, mshororo, mikondo, kituo, kikomo, mizani na kiwango⁴. Hivyo, ushairi unaweza kuwa ni utungo mfupi unaowasilisha mawazo kipicha. Aidha, unaweza kuimbwa au kughaniwa kwa mahadhi tofauti tofauti. Baadhi ya wataalamu wana mawazo kuwa, uwasilishaji wa ana kwa ana wa mashairi si lazima uimbwe kwa mahadhi ya kuvutia, bali kwa kuzingatia muktadha uliosawiriwa. Ni utanzu wenye maono unaoaniwasilishwa kwa lugha yenye mvuto na unaogusa hisi. Hata hivyo, swali ni: mvuto katika uwasilishaji wa mashairi hayo unatokana na sababu gani za kibinafsi? Ushairi ni aina ya utungo ambao huelezea hisi za ndani. Swali ni: ni hisia za aina na kwa kuzingatia mwelekeo gani? Huelezea hisi za ndani kwa kutumia lugha ya mkato au ufupi. Lugha ya mkato hapa pia ina utata, kwamba: ni ufupi wa mishororo au mawazo yanayowasilishwa? Kwa ambavyo ushairi wa hapo awali hasa katika miaka ya kabla ya 1960 yalitungwa na kuhifadhiwa kimoyomoyo au kuandikwa kwa nia ya kughaniwa au kuimbwa hadharani. Hii ndio sababu baadhi ya watunzi wa hapo awali (waliozingatia zaidi arudhi katika uwasilishaji mashairi yao hapo awali katika miaka ya 1980 kama vile S. A. Mohamed katika *'Sikate Tamaa* (1980) na *Kina cha Maisha* (1984) na baadaye alibadilisha mtindo wa uwasilishaji kwa kuzingatia mbinu za ushairi huru kama inavyoshuhudiwa katika *Jicho la Ndani* (2002).

³ Mahojiano yetu na Babusa ya tarehe 30.5. 2015) ambaye ni mhadhiri katika Idara ya Elimu na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Pia, ni mtunzi, mghanaji na mwimbaji wa mashairi ya Kiswahili yanayozingatia arudhi..

⁴ Huu ni mtazamo wa watunzi wengi ambao wanaoegemea zaidi katika mashairi ya kiarudhi katika jamii ya Waswahili.

Ushairi Huru wa Kiswahili katika Mkabala wa Ushairi Unaozingatia zaidi Arudhi

Kuzuka kwa ushairi huru kuliwawafanya watunzi maarufu wa ushairi wa kimapokeo kuungalia upya tungo zao na kuimarisha makali ya ala zao na waliweza kutunga tungo za kiwango cha juu cha usanii. Kwamba, vianzo vya ushairi na maendeleo yake ni mabadiliko ya kihistoria, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, migongano ya kitabaka katika jamii. Walianza kuzingatia msingi kuhusu utanzu na uwasilishaji na hasa kuhusisha masuala muhimu katika jamii. Walianza kuyapiga msasa mashiri hayo kwa kuyapa mtazamo mpya kulingana na mabadiliko katika jamii ambapo jamii zinahitajiana katika muktadha wa utandawazi. Kwa mantiki hii washairi wa kimapokeo iliegemea zaidi katika kuiwajibikia zaidi hadhira. Ushairi huru ulitokana na ushairi wa ndani na wala si nje ya muktadha unaofahamika wa Afrika Mashariki hivyo hakuna haja ya kuwa na mzozo na uadui wa kutoana na kujengeana uhasama. Shime ikawa ni kuwashajisha na kuwatia hamasa wasomaji na wasikilizaji kuukumbatia ushairi wao wa jadi badala ya kukimbilia ule mwingine. Kinachodhihirika ni kwamba, athari ya teknolojia na sayansi imeyafanya mashairi ya Kiswahili (hasa yale yanayowasilishwa kwa kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo) kupoteza uasili wake.

Hitimisho

Mashairi ya Kiswahili (yale yanaozingatia na yasiyozingatia zaidi arudhi katika utanzu na uwasilishaji) yanahitaji kulisukuma gurudumu la utanzu huu kwa njia moja inayofanana au kwa njia tofauti tofauti. Njia zote hizi zinazochangiana. Kimantiki, ugeni kwa mara ya kwanza unaogofya na unatuhumiwa. Hata hivyo, akili ya binadamu inahitaji kutayariishwa kwa utaratibu usiovunja. Wapenzi wa ushairi wa Kiswahili wajitolee katika usomaji wa kihakiki kwa kuzingatia utafiti ili kuweza kuufahamu zaidi ushairi wa Kiswahili. Matokeo yatakuwa ni kubainisha sura na sifa zake. Tofauti za kiutunzi katika makundi haya zinaweza kushirikishwa katika harakati za kufafanulia vipengele vya uwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Kwamba makundi yote mawili yanajenga nyumba moja (ingawa kwa njia tofauti) na hakuna haja ya kugombania fito.

Kwa wale wanaozingatia arudhi na utaratibu uliozoelewa miaka na mikaka hawana budi kuwa huru kujifunza mara kwa mara ili kunoa makali yao kutokana na yale yanaofanyika katika jamii zingine za kilimwengu. Kuna haja ya kutilia maanani hoja mbalimbali zinazotolewa kama njia ya kudhihirisha ukomavu wa ushairi huu kwa manufaa kizazi cha sasa na cha wakati ujao. Tuhuma za chini kwa chini zitachukua muda mrefu kabla maafikio ya dhati kuafikiwa. Ingawa watunzi wa mashairi huru walikuwa na maono kuhusu ushairi wa Kiswahili kwa ujumla; mwafaka huo utafikiwa lini iwapo muda mwingi utakuwa ni katika kutuhumiana? Kuna hatari ya kushika upande mwingine wa kijiti kusikostahili.

Ushairi huru wa Kiswahili ni wa kiwango cha juu kiuchambuzi na kiuhakiki ambapo unakuwa ni kichocheo na tafakari na chakula cha ubongo. Uwepo wa ushairi huru umekuwa ni kinoleo cha makali ya watunzi wa mashairi yanayozingatia zaidi arudhi katika uwasilishaji wake. Ujasiri wa watunzi wa mashairi huru umewafanya watu kuwa na mitazamo tofauti kuhusu fasili ya uhsiri wa Kiswahili. Tatizo lilikuwa ni namna watuzi hao walivyokuja kwa mikiki na mshindo kabla wanajamii hawajatayarishwa katika uitikio wa wapokezi. Mwanzoni katika miaka ya 1960, watunzi hao wa mashairi ya Kiswahili walisukumwa kwa mielekeo ya kutaka kutofautisha: ‘wa zamani’ na ‘kizazi cha kisasa’. Walipokuwa wakitunga katika miaka hiyo walikuwa vijana na hivi sasa ni wazee na ushairi wa Kiswahili bado upo na unatumwa katika mihadhara na katika maswala ya utafiti

Marejeleo

- Abdalla, A. (1973), *Diwani ya Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press
- Abdalla, A. (1978). “Wajibu wa Mshairi wa Kiswahili katika Jamii yake” katika *Zinduko*. Dar es Salaam: Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Achebe, C. (1973). “The Novelist as a Teacher” katika Killam, G. D. (Mh.) *African Writers on African Writing*. London: Heinemann.
- Adundo, (2014). ‘Athari ya Teknolojia katika Utanzu wa Ushairi’ katika *Taifa Leo*. Nairobi: Nationa Media Group.
- Alembi, E. (1999). *Understanding Poetry*. Nairobi: Acacia Publishers.
- Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi: Oxford University Press.
- Arege, T. I. M. (2014) *Fani ya Ushairi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Austin, J. (1962). *How to do Things with Words*. Clarendon: Oxford University Press.
- Barber, K. (1997). “Views of the Field.” in Barber (eds.) *Readings in African Popular Culture*. Oxford: James Currey.
- Chacha, C. N. (1980). “Ushairi wa Abdilatif Abdalla”, Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utezezi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Daiches, D. (1956). *Critical Approaches to Literature*. Eagleton Cliffs, N.J: Prentice-Hall Inc.
- Ezeliora, O. (2009). “Colonial Discourse, Poetic Language and the Igbo Masquerading Culture in Ezenwa Ohaetos: The Voice of the Night Masquerade”, katika *Journal of African Cultural Studies, Juzuu 21 na 1*. London: SOAS.

- Fanon, F. (1967). *Black Skins, White Masks*. New York: Grove Press.
- Fowler, R. (1966). "The Formulaic Theory and its Application to English Alliterative Poetry", katika Fowler, R. (Mh.), *Essays on Style and Language*. London: Routledge & Kegan.
- Gromov, M. D. (2006). "The Question of Kiswahili Style Again? The Poetry of Kithaka wa Mberia" katika *KISWAHILI Juzuu 69*. Dar es Salaam: TUKI.
- Harland, R. (1999). *Literary Theory from Plato to Barthes: An Introductory History*. New York: St. Martin's Press.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.
- Kezilahabi, E. (1983). 'Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili', katika *Makala ya Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Khatib, M. S. (1999). "Tamathali za Usemi", katika *MULIKA Na. 25*. Dar es Salaam: TUKI.
- M'Ngaruthi, T. K. (2012) *Miale ya Mashariki: Mashairi na Mwongozo wa Uchambuzi*. Ontario: Nsemia Inc. Publishers.
- Maitaria, J. N. (2015). "Sauti ya Kiharakati katika Ushairi wa Abdilatifu Abdalla", katika *Kiswahili na Maendeleo ya Jamii* M. Mukuthuria, J. O. Ontieri, M. Kandagor, and L. Sanja (wah.). Dar es Salaam: TATAKI (CHAKAMA), 193–210.
- Massamba, D. P. B. (1976). *Diwani ya Massamba*. Nairobi: Nelson East Africa
- Mathiora, J. na C. Mudachi (2007). *Reviving Poetry: Poetry Handbook for Secondary Students*. Nairobi Focus Publishers Ltd.
- Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*. Nairobi: East African Educational publishers.
- Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa*. Nairobi. Educational Research and Publications.
- Mohamed, S. A. (1984). *Kina cha Maisha*. Nairobi: Longhorn (K) Publishers Ltd.
- Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn (K) Publishers Ltd.
- Molefi, K. (1999). *The Painful Demise of Eurocentricism*. Trenton: N.J, African World Press Inc.
- Mulokozi M. M. na K. K. Kahigi (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M. (1978). "Ushairi wa Ukasuku", katika *Kioo cha Lugha*. Dar es Salaam. Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Ngure, A. (2014). 'Kinachofanya Shairi Lisomwe na Mvuto Maalum' katika *Taifa Leo uk. 21*. Nairobi: Nation Media Group

- Njogu, K. (2004). *Reading Poetry as Dialogue*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyanchama, M. B. (2004). "Matumizi ya Taswira na Istiara katika *Sauti ya Dhiki*", Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Nzuki, P. K. (2002). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Ohly, R. (1973). "Historical Approach to Swahili Literature. As Here to Fore an Open Question", katika *KISWAHILI Juz.Na. 43/2*. Dar es Salaam: TUKI.
- Said, A. M (2012). *Wasifu wa Ahmed Sheikh Nabhany*. London: JC Press
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia za Uihakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam university Press.
- Sharif, I. N. (1988). *Tungo Zetu: Msingi wa Mashairi na tungo nyinginezo*: New Jeasey: Readsea Press
- Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press
- Tolstoy, L. (1975). *What is Art*: Aylmer Maude (Mtaf.). London: Oxford University Press
- Wa Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publication Ltd.
- Wafula, R. M. na K. wa Njogu (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation
- Walibora, K. (2007). (Mhar). 'Utangulizi wa Mhariri' katika Diwani ya Karne Mpya. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Walibora, K. (2012) (Mhar). *Waja Leo*. Nairobi: Oxford University Press
- Wamitila, K. W. (2002). "Utangulizi" katika Mohamed S. A. *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn (Kenya) Ltd.
- Wangari, M. (2015). 'Sifa Bainifu za Mwandishi wa Kazi ya Kubuni' katika *Taifa Leo uk 21*. Nairobi: Nation Media Group.
- Wekesa, A. (2008). Mtindo katika Mashairi ya Diwani ya Karne Mpya. Tasnifu ya MA, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Zubkova-Bertoncini, E. (2008). "Some Remarks on Kithaka wa Mberia's Poetry", makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la 21st Century Swahili-Kolloquium, Chuo Kikuu cha Bayreuth.

